# Kupanua Ufikio wa Bima ya Afya kwa Wote

## (wakiwemo wahamiaji wasio na vibali!)

Kuanzia mwezi huu wa Novemba, kila mtu anayeishi katika jimbo la Washington atapata fursa ya kununua bima ya afya na meno kupitia *Washington Healthplanfinder*, bila kujali hali yake ya uhamiaji.

Jisajili ifikapo Des. 15 kwa bima ya afya inayoanza Jan. 1, 2024.

washington healthplanfinder
click. compare. covered.

## USTAHIKI, HALI YA UHAMIAJI, NA USALAMA

### Maneno Muhimu

**Ada ya Bima:** Kila mwanachama analipa ada ya kila mwezi inayoitwa "premium". Bei ya "premium" yako inategemea na aina ya bima yako ya afya.

**Makato:** Bima yako ya afya inaanza kukusaidia kulipia bili zako baada ya "kufikia kiasi chako cha makato". Bima zote zinalipia matibabu ya kinga kabla kipindi cha makato yako hakijafikiwa. **Bima za Cascade Care** zinalipia huduma zaidi kabla kipindi cha makato yako hakijafikiwa. Huduma hizi zinajumuisha:

- Matibabu ya kinga
- Matibabu ya msingi, kumwona daktari kwa ajili ya ugonjwa au jeraha
- Huduma za afya ya akili
- Kuandikiwa dawa za kawaida
- Matibabu ya haraka, ukihitaji matibabu ya haraka mara moja lakini huna dharura kama shambulio la moyo.

**Malipo shirikishi na bima shirikishi:** Hizi ni gharama unazolipa ukienda kwa daktari. Malipo yako shirikishi ni kiasi kisichobadilika ($1-$50). Bima yako shirikishi ni asilimia ya gharama ya huduma. Aina yako ya bima ya afya inalipia ziara yote ya kumwona daktari.

### Nani ana ustahiki?

Ikiwa unaishi katika jimbo la Washington, unaweza kununua bima ya afya kupitia *Washington Healthplanfinder*, hata kama wewe ni mhamiaji usiye na vibali. Huhitaji uraia wa Marekani, "green card", au nyaraka nyingine za uhamiaji.

### Je, kuwa na bima ya taifa kutaathiri hali yangu ya uhamiaji au maombi yangu ya uraia?

Kupata bima ya afya hakuathiri hali yako ya uhamiaji au maombi ya uraia kwa ajili yako, familia yako, au yeyote anayeishi pamoja nawe.

### Je, kuwa na bima ya taifa kutanifanya kuwa "tegemezi kwa serikali"?

Kutuma maombi au kupata bima ya afya, na kupata usaidizi wa kifedha ili kulipia bima, haimfanyi mtu kuwa "tegemezi kwa serikali". Hii inamaanisha haitaathiri hali ya uhamiaji au maombi ya uraia kwa ajili yako, familia yako, au yeyote anayeishi pamoja nawe.

### Sina vibali. Je, taarifa zangu zipo salama?

Usalama wako ni muhimu kwetu. **Taarifa zako hazitatumika kwa ajili ya ushurutishaji wa uhamiaji.**

Sheria za serikali kuu na za jimbo zinalinda faragha ya watu wanaotuma maombi ya bima ya afya kupitia *Washington Healthplanfinder*. Taarifa kuhusu hali ya uhamiaji zitatumika tu kubaini ustahiki wa kupata bima na si kwa ajili ya ushurutishaji wa uhamiaji.

# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

## KUJIANDIKISHA

### “Kujiandikisha” ni nini?

Unajiandikisha kwenye bima ya afya kwa kuchagua aina ya bima kupitia *Washington Healthplanfinder*, na kisha kuilipia bima yako.

### Lini naweza kujiandikisha? “Kipindi cha uandikishaji” ni nini?

Yeyote anaweza kujisajili kwa ajili ya bima ya afya kupitia *Washington Healthplanfinder kati* ya **Nov. 1 na Jan. 15**. Kipindi hiki kinaitwa **kipindi cha uandikishaji**. Kipindi hiki cha uandikishaji hufanyika kila mwaka.

### Vipi kama nikikosa kipindi cha uandikishaji? “Kipindi maalum cha uandikishaji” ni nini?

Baadhi ya watu wanaweza kuajindikisha wakati mwingine. Hii inaitwa **kipindi maalum cha uandikishaji**.

Ukiwa na mabadiliko ya kimaisha (kupoteza ajira, mabadiliko katika ndoa, kuzaliwa kwa mtoto, nk.) au ni mwenye kipato kidogo, unaweza kujiandikisha nje ya kipindi cha uandikishaji.

### Nitahitaji nini ili kujiandikisha?

*Washington Healthplanfinder* itaomba taarifa kuhusu wewe na familia yako ili kubaini ustahiki wenu.

### Itachukua muda gani?

Maombi yanaweza kuchukua takribani lisaa 1.

### Wapi naweza kupata usaidizi kuhusu kujiandikisha? Kuna usaidizi unaopatikana kwa lugha nyingine?

Usaidizi wote wa kuajindikisha ni **bure***. Hizi hapa ni njia tatu za kupata msaada:

**Piga**

1-855-923-4633
TTY/TDD: 1-855-627-9604

*Msaada unapatikana kwa lugha zaidi ya 200.*

**Wasiliana**

**Weka miadi** na ‘navigator, broker’ wa fya au chanzo cha kuaminika katika jumuiya yako.

**Tembelea**

www.wahealthplanfinder.org

*au tambaza msimbo wa QR kupitia kamera yako*

**Ili kutazama aina za bima katika eneo lako, tembelea wahealthplanfinder.org.** Tumia zana ya “Browse and Compare Plans”.

*Ikiwa hujui iwapo mtu fulani ameidhinishwa kukupa usaidizi, au akiomba kulipwa kwa huduma zake, wapigie Kituo cha Usaidizi kwa Wateja cha *Washington Healthplanfinder* kupitia **1-855-WAFINDER**.



# Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

## GHARAMA YA BIMA YA AFYA

### Bima ya afya inagharimu kiasi gani?

Gharama ya kununua bima ya afya inategemea na vitu kama kipato chako, ukubwa wa familia, na mahali unapoishi.
Peruzi na linganisha aina za bima kwenye **wahealthplanfinder.org** au shirikiana na chanzo cha kuaminika katika jumuiya yako kufahamu bima itakugharimu kiasi gani.

### Maneno haya yanamaanisha nini: ada ya bima (premium), makato (deductibe), bima shirikishi (co-insurance) na malipo shirikishi (co-pay)?

**Ada ya Bima:** Kila mwanachama analipa ada ya kila mwezi inayoitwa "premium". Bei ya "premium" yako inategemea na aina ya bima yako ya afya.

**Makato:** Bima yako ya afya inaanza kukusaidia kulipia bili zako baada ya "kufikia kiasi chako cha makato". Bima zote zinalipia huduma fulani, kama ukaguzi wa kiafya, kabla kipindi cha makato hakijafikiwa.

**Malipo shirikishi na Bima shirikishi:** Hizi ni gharama unazolipa ukienda kwa daktari. Malipo yako shirikishi ni kiasi kisichobadilika ($1-$50). Bima yako shirikishi ni asilimia ya gharama ya huduma. Aina yako ya bima ya afya inalipia ziara yote ya kumwona daktari.

### "Gharama kutoka mfukoni" ni nini?

Gharama kutoka mfukoni (makato, malipo shirikishi, na bima shirikishi) hurejelea kiasi unacholipa ukienda kwa daktari.

## KUCHAGUA AINA YA BIMA

### Aina gani za bima za afya zinapatikana?

Kuna ngazi tatu za bima za afya zinazopatikana kupitia *Washington Healthplanfinder*: Shaba, Fedha, na Dhahabu.

Kiasi kinacholipwa na kampuni yako ya bima ya afya kinategemea na ngazi gani unachagua. Kwa wastani, ngazi ya Shaba inalipa takribani 60%, ngazi ya Fedha inalipa takribani 70%, na ngazi ya Dhahabu inalipa takribani 80% ya bili zako za matibabu.

**Shaba:** Bima hizi zinagharimu kidogo zaidi kwa mwezi lakini zinalipia gharama kidogo unapohitaji matibabu.

**Fedha:** Bima hizi zinakinga zaidi ya gharama zako ukihitaji matibabu lakini zinaweza kugharimu zaidi. Ukifuzu Cascade Care Savings bima hizi zinaweza kugharimu kidogo zaidi kuliko bima za Shaba.

**Dhahabu:** Bima hizi zinagharimu zaidi kwa mwezi lakini zinalipia gharama zaidi ukihitaji matibabu. Ukifuzu Cascade Care Savings na una mahitaji makubwa ya huduma ya afya bima hizi zinaweza kukufaa zaidi.

### Nitapata madaktari bora nikichagua bima za Fedha au Dhahabu?

Hapana. Ubora wa matibabu ni ule ule kwa bima zote.

washington healthplanfinder
click. compare. covered.

**Angalia nembo ya Cascade Care.**
Bima za Cascade Care zinatoa thamani zaidi kwa gharama ndogo. Yaani, malipo yako ya ada ya bima yanakupa faida zaidi!

CASCADE CARE